

Wakati nilipokuwa na miaka kumi na tano, wazazi wangu na mimi tulitembelea ziwa la Tanganyika lililopo katika mpaka wa nchi za Tanzania na Kongo. Ilikuwa safari ndefu. Tulianza mjini Arusha, na tulipita sehemu nyingi kufikia Kigoma. Siku ya kwanza, tulipita Bonde la Ufa, na Ngorongoro kufikia mbuga ya wanyama ya Serengeti. Tulikaa Serengeti hotelini, labda huko ziwa la Ndotu au Seronera; sikumbuki vizuri.

Siku iliyofuata, tulisafiri Mwanza. Ilikuwa safari nzuri sana. Tuliona wanyama wengi na mandhari nzuri kabisa. Tulipofika Mwanza, tulikaa hotelini. Tuliuliza hotelini tungehitaji muda gani kufikia Kigoma kutoka Mwanza. Tuliambiwa labda siku moja. Tulifikiri hivyo pia. Umbali kati ya Mwanza na Kigoma takriban ni sawasawa na ule kati ya Arusha na Dar.



Michuzi)

Kivuko (Picha kutoka tovuti ya Issa

Basi, mapema asubuhi iliyofuata, tulikisubiri kivuko ili tuvuke ziwa. Tulivushwa, tukaanza tena safari. Tuliendelea barabarani kwa siku nzima. Lakini, wakati usiku ulipofika, bado tulikuwa mbali sana na Kigoma. Hata hatukujua tulipo. Tulisafiri na tulisafiri. Kulikuwa na mashimo makubwa barabarani. Mara moja tuliona tundu ambayo gari letu lingeweza kuingia ndani yake kabisa. Ilikuwa si wazo zuri kuendesha usiku, lakini hatukuona pahala pa kukaa. Kama saa sita, tuliona kundi la watu barabarani. Tulijadiliana kidogo hatari ya kusimamisha gari, halafu tuliamua kwa tahadhari kusimama, kuteremsha kioo na kuuliza tuko wapi. Pahala panaitwaje? Nadhani hawakuelewa neno lolote la kiswahili potofu chetu. Waliogopa, wakakimbia kwa kasi kubwa kabisa.

Tuliendelea. Alfajiri ilifika, na mwishowe tuliwasili hoteli ya Kigoma saa kumi na moja. Kwa bahati, hatukuishiwa na petroli. Tulipumzika kidogo tukaondoka tena kwa boti kwa safari ya takriban masaa kumi mengine, kufikia mbuga ya Milima ya Mahale. Tulikaa huko kwa siku kadhaa, na tulirudi Arusha. Safari ya kurudi ilikuwa refu sana pia. Lakini badala ya kupita Mwanza tulipita miji ya Nzega na Singida.

hadithichad.mp3